**MULIKA Na. 44(2) DESEMBA 2025**

# JARIDA LA TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI

**MHARIRI MKUU**
**Titus Mpemba**

**MHARIRI MSAIDIZI**
**Edith Lyimo**

**ISSN 0856-0129**
**e-ISSN 2546-2202**

©TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI 2023

**Mhariri Mkuu**
Dkt. Titus Mpemba, Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, titus.mpemba@udsm.ac.tz; mpembatitus@gmail.com

**Mhariri Msaidizi**
Dkt Dkt. Edith B. Lyimo, Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam edithbalyimo@gmail.com

**Bodi ya Uhariri**
Dkt. Titus Mpemba, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania
titus.mpemba@udsm.ac.tz; mpembatitus@gmail.com
Dkt. Edith B. Lyimo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania
edithbalyimo@gmail.com
Dkt. Ramadhani T. Kadallah, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania
Kadallahr@yahoo.com
Prof. Shani O. Mchepange, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania
shaniom@yahoo.co.uk
Dkt. Lutz Diegner, Chuo Kikuu cha Humboldt, Ujerumani
lutz.diegner@asa.hu-berlin.de
Dkt. Athumani Ponera, Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania
atponeraman@gmail.com
Dkt. Miriam Kenyani Osore, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya
kenyanimo@yahoo.com

**Washauri wa Wahariri**
Prof. Abdulaziz Lodhi, Chuo Kikuu cha Uppsala, Sweden
Abdulaziz.lodhi@lingfil.uu.se
Prof. Sangai Mohochi, Chuo Kikuu cha Kibabii, Kenya
smohochi@gmail.com
Prof. Cyprean Niyomugabo, Chuo Kikuu cha Rwanda
niyomugabocyprien@gmail.com
Prof. Method Samwel Semiono, Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa, Tanzania
methodsamwel16@gmail.com
Prof. Ipara Odeo, Chuo Kikuu cha Kibabii, Kenya
iodeo@kibu.ac.ke
Prof. Alwiya Saleh Omar, Chuo Kikuu cha Indiana, Bloomington-Marekani
alwiyahuseina@gmail.com
Prof. Beata Wojtowicz, Chuo Kikuu cha Warsaw, Poland
b.wojtowicz@uw.edu.pl
Dkt. Wael Nabil Ibrahim, Chuo Kikuu cha Al Azhar, Misri
wael_nibrahim@hotmail.com
Dkt. Felix Kwame Sosoo, Chuo Kikuu cha Ghana, Ghana
munguananipenda@yahoo.com

**ADA KWA MWAKA**[1]

| | |
|---|---|
| Kwa Taasisi | US $ 40 pamoja na usafiri |
| Kwa Mtu Binafsi | US $ 20 pamoja na usafiri |
| Jina la Akaunti | University of Dar es Salaam |
| Namba ya Akaunti | 012105005554 |
| Jina la Benki | National Bank of Commerce |
| Tawi la Benki | UDSM Branch |
| Msimbo wa Benki | 255 |
| Msimbo wa Utambulisho | NLCBTZTX |
| Bei ya Jarida kwa Tanzania | ShT 10,000 |

**Habari za Mkondoni**

Makala katika jarida hili yanapatikana pia katika tovuti za www.udsm.ac.tz; www.ajol.info na https://mft.ebscohost.com.

**Kwa mawasiliano tumia anwani ifuatayo:**
**Mhariri Mkuu, MULIKA**
**Taasisi ya Taaluma za Kiswahili-Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,**
**S.L.P. 35110**,
**Dar es Salaam**.
Baruapepe: mulika1970@udsm.ac.tz; mulika.udsm@gmail.com

**Hakimiliki**

Hakimiliki © Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa wala kutoa makala ya jarida hili kwa njia yoyote ile bila idhini ya mchapishaji, isipokuwa kwa nukuu fupi kwa ajili ya utafiti au matumizi binafsi, mapitio ya kitaaluma au mjadala kwa kuwarejelea waandishi wa makala husika.

[1] Ada hizi ni kwa nakala ngumu kwani nakala tepe zinapatikana bila malipo.

# Taarifa kwa Waandishi wa Makala

## Usuli na Mawanda

*MULIKA* ni jarida la taaluma ya lugha na fasihi ya Kiswahili. Jukumu lake kuu ni kukusanya na kusambaza maarifa yanayohusu lugha na fasihi ya Kiswahili yaliyokitwa katika utafiti mpevu. Kutokana na mahitaji kwa baadhi ya watumiaji wa Kiswahili katika nyanja nyingine, hivi sasa jarida hili linapokea pia makala zilizoandikwa kwa lugha ya Kiswahili lakini zenye maudhui mengine nje ya lugha na fasihi ya Kiswahili. *MULIKA* limeendelea kuwa daraja kati ya watumiaji wa Kiswahili popote walipo, na wataalamu wa Kiswahili katika shule za sekondari na vyuo vya elimu ya juu Afrika ya Mashariki na kwingineko.

## Uandaaji na Utumaji wa Makala

Jarida linapokea makala zilizoandikwa kwa Kiswahili TU. Makala hizo zinapaswa zipigwe chapa kwa mfumo wa *Microsoft Word*, mistari ikitengwa kwa kipimo cha nafasi ya 1.5 baina ya mstari na mstari, na pambizo liwe na upana toshelevu, angalau sentimeta 2.5. Ukurasa wa kwanza wa makala uoneshe jina la makala, jina kamili la mwandishi (au waandishi) wa makala (ikiwa ni pamoja na wadhifa wake), anwani, na baruapepe yake. Ukurasa wa pili uoneshe jina la makala na ikisiri isiyozidi maneno 200. Makala iwe na maneno 4000-8000 na mapitio ya vitabu yawe na maneno 800-1200.

## Upitiaji na Uhariri wa Makala

Makala yoyote, kabla ya kuwasilishwa, inatakiwa iwe imepitiwa vyema na mwandishi na kufanyiwa uhariri wa kina ili kuhakikisha kwamba haina makosa ya kiuandishi na kimaudhui. Mwandishi anapaswa pia kuhakikisha kwamba taarifa zote zilizomo ndani ya makala ni sahihi na vyanzo vya taarifa hizo ni vya kuaminika.

## Urejeleaji

Unapotaja marejeleo kwenye matini, taja jina la mwisho la mwandishi likifuatiwa, katika mabano, na mwaka wa kuchapishwa kwake na kurasa zilizorejelewa, k.m. Yahya (1983:139). Kwenye orodha ya marejeleo au bibliografia, majina ya warejelewa yapangwe kialfabeti. Tanchini na tanmwisho ziwekwe namba na zitumike pale inapobidi tu. Maelezo ya tanmwisho yatolewe kwenye ukurasa wa peke yake mwishoni mwa makala kabla ya kuorodhesha marejeleo.

Majina ya vitabu, majarida, na anwani za tasnifu/tazmili viandikwe kwa *hatimlazo*. Majina ya makala yawekwe ndani ya alama za kufunga na kufungua semi. Kwa uangavu zaidi, tazama mifano ifuatayo:

**Kitabu (Mwandishi Mmoja)**

Massamba, D.P.B. (2017) *Historia ya Kiswahili: Mtazamo Mpya 100 KK hadi 2000 BK*. Dar es Salaam: Kiswahili Development Limited.

**Kitabu (Waandishi Zaidi ya Mmoja)**

Mazrui, A.A. na Mazrui, A.M. (1995) *Swahili State and Society: The Political Economy of an African Language.* Nairobi: James Currey

**Sura ya Kitabu**

Hamisi, A.M. (2008) "Filosofia za Sera za Lugha". Katika J.G. Kiango (Mh.) *Maendeleo ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI. kur. 78-100.

**Makala ya Jarida**

Majariwa, D. (2021) "Upenyezaji na Ukubalifu wa Mkururo wa Konsonanti katika Fonolojia ya Kiswahili: Mifano katika Maneno Yaliyopokelewa kutoka Kiingereza na Kiarabu". *Mulika*, Juz. Na. 40 (1): 1-23.

**Makala ya Jarida la Mkondoni**

Omari, S. (2019) "Gender Representation in Simba and Yanga's Joking Cartoons in Tanzania". *Eastern African Literary and Cultural Studies*. Juz. 5(2): 79-93. Inapatikana katika https://doi.org/10.1080/23277408.2019.1643606. Ilisomwa tarehe 12 Juni 2012.

**Tasnifu/Tazmili Isiyochapishwa**

Peterson, R. (2014) *Matumizi na Dhima za Lugha katika Mandhari-lugha ya Jiji la Dar es Salaam*. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Saalam.

**Gazeti**

Duwe, E. (2018) "Zijue Sifa za Kufundisha Kiswahili Nje ya Nchi". *Mwananchi*. 16 Oktoba 2018. uk. 13.

## Mifano na Vielelezo Ndani ya Makala

Mifano, majedwali, michoro, ramani na picha zote vipangwe kwa uwazi na unadhifu kwenye kila ukurasa kadiri vilivyotumika. Taarifa zote hizo zinapaswa kutumika kwa kuzingatia kanuni za maadili ya kazi ya kitaaluma. Mathalani, ni muhimu kuweka chanzo thabiti cha taarifa inayoingizwa kwenye makala, iwe ni picha, michoro, mifano na vingine vinavyohusiana na hivyo. Kwa ujumla, data zinazotumiwa katika makala ni lazima ziwe thabiti na zenye kuaminika.

## Ubwakuzi wa Kitaaluma

Kunakili maneno, mawazo, michoro, n.k., kutoka vyanzo vingine bila kubainisha vyanzo husika kutafasiriwa kuwa ni ubwakuzi wa kitaaluma na hiyo inaweza kuwa miongoni mwa sababu za makala yako kukataliwa. Ikiwa itabainika kuwa makala iliyochapishwa katika jarida imekiuka maadili ya kazi za kitaaluma, taratibu za kisheria zitachukuliwa kwa mujibu wa kanuni na miongozo iliyopo.

## Ridhaa ya Kuchapisha

Ikiwa makala itakubaliwa, mwandishi wa makala ataandikiwa barua kupewa

taarifa hiyo. Mwandishi wa makala atapaswa kuthibitisha kwa maandishi kwamba makala hiyo haijachapishwa wala kutumwa mahali pengine. Taarifa hiyo itachukuliwa kuwa ni idhini ya makala hiyo kuchapishwa katika Jarida la *MULIKA*.

**Mchakato wa Kutathmini Makala**

Makala za *MULIKA* zitatathminiwa na wasomaji wasiopungua wawili ambao watafanya kazi hiyo bila kufahamu taarifa za mwandishi. Waandishi wanatakiwa kuepuka kuonesha utambulisho wowote unaowahusu ndani ya makala ili kuwawezesha wanaoitathmini kufanya kazi yao kwa haki. Sifa mojawapo ya watu watakaotathmini makala ni weledi katika uga unaofanyiwa tathmini. Mbali na kutumwa kwa watu wa kutathmini, makala itapitiwa pia na wahariri wa jarida ili kuhakikisha kwamba imetimiza mahitaji ya jarida kabla ya kuendelea na hatua inayofuata.

Miongoni mwa vipengele vitakavyozingatiwa wakati wa kutathmini makala ni walengwa wa makala, lengo la makala, mapitio ya maandiko, nadharia, mpangilio na uwasilishaji, ufafanuzi wa maudhui, uasili na uzingatiaji wa maadili, matumizi ya michoro na picha, uandishi wa matini na marejeleo.

Endapo maudhui ya makala yatakidhi mawanda na sera za jarida, makala itatumwa kwa watathmini wawili ambao hawajulikani kwa mwandishi, kuwaomba kukubali kuitathmini makala. Watathmini watatathmini miswada wakilenga kuangalia ubora wake katika maudhui, uwazi wa uwasilishaji, uasili, mchango wake kitaaluma na uzito wake kimaudhui na kiutafiti. Watathmini watapatiwa mwongozo utakaowaongoza wakati wa kutathmini makala. Baada ya kupata maoni ya watathmni, wahariri watapitia maoni hayo kabla ya kuyatuma kwa waandishi wa makala ili kuhakikisha kwamba maoni yaliyotolewa yanaendana na mwongozo uliotolewa. Baada ya maoni hayo kupitiwa na wahariri kujiridhisha kwamba yanaendana na mwongozo wa jarida, yatatumwa kwa mwandishi wa makala ili ayafanyie kazi kisha kurejesha muswada uliozingatia maoni yaliyotolewa na watathmini wa makala. Wakati wa kurejesha makala baada ya kufanyia kazi maoni, mwandishi wa makala atapaswa kuandaa jedwali linaloonesha maoni aliyopewa na namna alivyoyafanyia kazi.

Kutozingatia mwongozo wakati wa kuandaa makala kunaweza kuwa sababu ya makala kutopewa nafasi katika hatua za awali za tathmini. Aidha, kutozingatia makataa ya kufanya marekebisho kwa waandishi wa makala kunaweza kuwa sababu ya makala zao kutozingatiwa katika toleo husika.

Waandishi ambao makala zao zitakubaliwa, mbali na kuandikiwa barua kujuzwa hatua ya kukubaliwa kwa makala hizo, watatumiwa nakala tepe za makala zao

pamoja na kurasa za awali zinazoonesha taarifa mbalimbali za jarida kwa marejeleo.

Jambo muhimu la kuzingatia ni kwamba maoni yaliyomo kwenye makala yaliyochapishwa katika jarida hili ni ya waandishi wa makala na si lazima yakubaliane na yale ya Wahariri au Bodi ya Uhariri ya Jarida la *Mulika* na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili kwa ujumla wake.

# YALIYOMO

**UKURASA**

Taarifa kwa Waandishi wa Makala............................................................ v

Tahariri.......................................................................................... x

Waandishi wa Makala...................................................................... xii

Uchunguzi wa Maumbo ya Wingi wa Heshima kwenye Kategoria za Kileksika za Lugha ya Kimatengo
*Fokas Nchimbi*………………………………………………………… 153

Utumwa wa Kimaandishi na Kupuuzwa kwa Turathi Simulizi za Mwafrika: Uchunguzi Kifani wa Ukalimani wa Lugha ya Mizimu
*Titus Mpemba*.................................................................................. 172

Uundaji wa Maneno ya Kiswahili katika Mawasiliano Mahalia: Utafiti wa Lugha za Kundi F30
*Rehema Stephani*……………………………………………………… 188

Uamilifu wa Mofu {(-)i-} katika Kiswahili Kinachozungumzwa nchini Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo
*Dieudonné Butoyi na Anitha Nduwamahoro*................................................ 209

Sababu za Kuibuka kwa Uchapishaji-binafsi wa Kazi za Fasihi Andishi ya Kiswahili Nchini Tanzania
*Erasto Duwe, Angelus Mnenuka, na Leonard Bakize*.................................. 227

Wahusika wa Kivisasili na Athari yake katika Riwaya ya Kiswahili
*Rose Jackson Mbijima*.................................................................... 248

Usawiri wa Wahusika wa Ajabuajabu katika Riwaya Teule za Kihalisiajabu za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi
*Charles Nyanduru Maggati*............................................................... 268

Urudiaji wa Kisufi na Motifu kama Mtindo Katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*
*Aloo Ronald Odhiambo na Kineene wa Mutiso*........................................... 291

Uchunguzi wa Mandhari katika Ujenzi wa Usaliti: Mifano kutoka Diwani ya *Wasakatonge* ya M. S. Khatib
*Baraka Sikuomba na Shani Omari Mchepange*............................................ 313

## TAHARIRI

Wapendwa Wasomaji,

Kwa mara nyingine, Jarida la *Mulika* linawaletea tena mkusanyiko wa makala mbalimbali kupitia Juzuu Na. 44 (2), toleo la Desemba 2025. Katika toleo hili, kuna jumla ya makala 9 (tisa) kuhusu nyuga mbalimbali za taaluma za Kiswahili. Kimahususi, miongoni mwazo, makala 5 (tano) zinaangazia uga wa fasihi na makala 4 (nne) zimejikita katika uga wa isimu. Tunawakaribisheni mzisome makala hizi kitunduizi ili kuyaelewa kwa kina yaliyomo na kutoa maoni stahiki pale inapobidi.

Tukianza na uga wa isimu, makala ya Fokas Nchimbi inachunguza maumbo ya wingi wa heshima katika lugha ya Kimatengo kwa kuangalia uwasilishaji wake katika kategoria mbalimbali za kileksika. Kwa kutumia Nadharia ya Upole, makala hii inaonesha kuwa wingi wa heshima ni dhana ya kiisimujamii inayodhihirika katika nomino, viwakilishi, vivumishi, na vitenzi kwa kuzingatia hadhi ya mhusika katika jamii. Makala ya Titus Mpemba inajadili dhana ya utumwa wa kimaandishi na kupuuzwa kwa turathi simulizi za Mwafrika kwa kurejelea ukalimani wa lugha ya mizimu. Makala hii inaonesha kuwa maarifa yasiyoandikwa yana hadhi sawa na yale ya maandishi na kwamba ukalimani huo una sifa zote za ukalimani wa kisasa. Aidha, makala ya Rehema Stephano inahusu uundaji wa maneno ya Kiswahili katika mawasiliano mahalia ya jamii za Kundi F30. Matokeo yanaonesha kuwa uundaji huo hufuata kanuni za unasibu, utohoaji, uhamishaji, na ukarabati-maana ili kukidhi mahitaji ya mawasiliano. Vilevile, kuna makala ya Dieudonné Butoyi na Anitha Nduwamahoro ambayo inachambua uamilifu wa mofu {(-)i-} katika Kiswahili kinachozungumzwa Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Makala hii inaonesha kuwa mofu hiyo ina uamilifu mpana wa kimofosintaksia na inaweza kuwakilisha ngeli mbalimbali bila kuzingatia idadi.

Kwa upande wa uga wa fasihi, makala ya Erasto Duwe, Angelus Mnenuka, na Leonard Bakize inachunguza sababu za kuibuka kwa uchapishaji-binafsi wa kazi za fasihi andishi ya Kiswahili nchini Tanzania. Makala hii inaonesha kuwa hali hiyo imesababishwa na changamoto za kiuchumi, mifumo ya uchapishaji yenye vikwazo, na mabadiliko ya mahitaji ya waandishi. Makala ya Rose Jackson Mbijima inahusu wahusika wa kivisasili na athari zake katika riwaya za Kiswahili. Matokeo yanaonesha kuwa wahusika hao huchangia katika urithishaji wa amali za kiutamaduni,

uunganishaji wa ujadi na usasa pamoja na utambulishaji wa jamii. Makala ya Charles Nyanduru Maggati inachunguza usawiri wa wahusika wa ajabuajabu katika riwaya teule za kihalisiajabu, ikionesha kuwa wahusika hao hutumika kusawiri hali halisi za jamii kwa mbinu za kifasihi. Aidha, makala ya Aloo Ronald Odhiambo na Kineene wa Mutiso inachambua urudiaji wa kisufi na motifu kama mtindo katika utenzi wa *Seyidina Ali* na *Mudhari bin Darimi*, na kubainisha kuwa urudiaji huo ni msingi wa ujenzi wa fani na maudhui. Mwisho, makala ya Baraka Sikuomba na Shani Omari Mchepange inachunguza nafasi ya mandhari katika ujenzi wa usaliti katika diwani ya *Wasakatonge*, ikionesha kuwa mandhari hutumika kujenga na kufichua matendo ya usaliti katika miktadha mbalimbali ya kijamii.

Kwa ujumla, makala hizi zinaonesha mwelekeo mpana wa tafiti za Kiswahili katika nyanja za isimu na fasihi, zikidhihirisha mchango wa taaluma hizi katika kuchambua lugha, jamii, na utamaduni. Ni matumaini ya wahariri kwamba mtanufaika na maarifa yaliyomo na kuendelea kushiriki katika kuendeleza taaluma za Kiswahili kwa kuandika na kuchapisha makala katika jarida hili. Karibuni sana tuzisome na kuzitafakari makala hizi kwa furaha.

*Wahariri, Desemba 2025*

## WAANDISHI WA MAKALA MULIKA NA. 44 (2)

| Na. | Jina | Taasisi |
|---|---|---|
| 1 | Fokas Nchimbi | Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam |
| 2 | Titus Mpemba | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam |
| 3 | Rehema Stephano | Chuo Kikuu cha Dodoma |
| 4 | Dieudonné Butoyi na Anitha Nduwamahoro | Chuo Kikuu cha Burudni |
| 5 | Erasto Duwe, Angelus Mnenuka na Leonard Bakize | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam |
| 6 | Rose Jackson Mbijima | Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam |
| 7 | Charles Nyanduru Maggati | Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam |
| 8 | Aloo Ronald Odhiambo na Kineene wa Mutiso | Chuo Kikuu cha Nairobi |
| 9 | Baraka Sikuomba na Shani Omari Mchepange | Chuo Kikuu Kishiriki cha Marian na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam |